

JARIDA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI,
SANAA NA MICHEZO

Jarida La Mtandaoni **Toleo la. 09** | 27 MEI, 2021

www.habari.go.tz



Wizara HabariTz



Wizara_habaritz



Wizara_HabariTZ

TAHARIRI

RAIS SAMIA ATOA MAELEKEZO KWA MAAFISA HABARI NCHINI

Hivi karibuni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ametoa salamu na maelekezo mahususi kwa Maafisa Habari, Mawasiliano, Uhusiano na Itifaki kwenye ufunguzi wa kikao kazi cha 16 cha Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano (TAGCO) Jijini Mbeya.

Amesema “Muendeleo kuhimizana umuhimu wa taarifa za kazi zenu kwa umma, yale mazuri au hata yasiyoridhisha lazima kuwe na namna ya kutoa taarifa kwa umma. Msiache mpaka wananchi wanaolalamika na kudai kuelezwa lililopo ndio taarifa inatolewa. Vinginevyo nawatakia mkutano mwema na kazi iendelee”.

Ni ukweli usioplingika kuwa katika zama za sasa endapo taaluma ya habari ikitumika kimkakati itasaidia kutimiza malengo ya Serikali.

Tunafurahi kuona kuwa katika kuhitimisha kikao hiki wanachama walijadili namna bora ya kutekeleza maelekezo hayo ya Mhe. Rais na hotuba ya Waziri Bashungwa chini ya uenyekiti wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari Dkt. Hassan Abbasi na kuahidi kuyafanyia kazi kikamilifu.

Tunachukua nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais kwa kutambua mchango wa Maafisa Habari, Mawasiliano, Uhusiano na Itifaki serikalini katika kuelezea shughuli mbalimbali za Serikali. Tunaamimi maelekezo haya ni chachu na mwanzo mpya wa ufanisi wa kazi kwa Maafisa Habari katika kuisemea Serikali.

Sisi Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo tunaona kauli ya Mhe. Rais imeitoka katika wakati mwafaka ambapo Serikali inafanya mambo mengi yanayopaswa kupelekwa kwa wananchi ili wafahamu, waiamini, waikubali na washiriki kikamilifu katika kutekeleza hatimaye kujenga uchumi imara wa nchi yetu.

Tunapongeza jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara chini ya Mhe. Waziri Innocent Lugha Bashungwa (Mb), Naibu wake Pauline Gekul (Mb) na Menejimenti ya Wizara ikiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Hassan Abbasi na Naibu wake Dkt. Ally Possi kwa kutoa miongozo na usimamizi thabiti wa Sera na maelekezo mbalimbali ya viongozi Wakuu wa nchi.

Kwa upande mwingine tunatoa pongezi za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara yetu Dkt. Hassan Abbasi kwa tunukiwa tuzo ya pongezi na TAGCO kwa mchango na mageuzi makubwa aliyoyaleta katika kipindi chake akiwa kwenye nafasi ya Mkurugenzi wa Idara ya Habari -MAELEZO na Msemaji wa Serikali.

Tunaungana na kauli ya Mhe. Rais, maelekezo yake pamoja na salamu inayosisitiza kuiheshimu na kuipenda nchi yetu kwa kusema “Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kazi lendelee.”



UJUMBE WA MHE. RAIS SAMIA SULUHU HASSAN KATIKA KIKAO KAZI CHA 16 CHA MAAFISA HABARI, MAWASILIANO NA UHUSIANO WA SERIKALI

“Naona muendeleo kuhimizana umuhimu wa taarifa za kazi zenu kwa umma, yale mazuri au hata yasiyoridhisha lazima kuwe na namna ya kutoa taarifa kwa umma.

Wasiache mpaka wananchi wanalalamika na kudai kuelezwa lililopo Ndio taarifa inatolewa.

Vyenginevyo nawatakia mkutano mwema na kazi iendeleo”





WIZARA YA HABARI NA MALIASILI KUSHIRIKIANA KUTAMBUA MAENEO YA URITHI NA KUYALINDA

Na Shamimu Nyaki, DAR ES SALAAM

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa amezitaka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Wizara ya Maliasili na Utalii kushirikiana katika kuyatambua maeneo ya urithi yanayokidhi vigezo vya kuingizwa katika Gazeti la Serikali na kuwa urithi wa Taifa ili yalindwe Kisheria.

Waziri Mkuu amesema hayo Mei 21, 2021 Jijini Dar es Salaam alipofungua Kongamano la Kutambua na Kuenzi Mchango Anuwai wa Historia ya Tanzania katika Ukombozi wa Bara la Afrika ambapo amewasisitiza Watanzania kujivunia historia hiyo kwa kufanya kazi kwa bidii na kulinda rasilimali za nchi kwa uzalendo, kuendelea kuwa na Utangamano, Utaifa pamoja na kuenzi mazuri yaliyoachwa na wapigania Uhuru wa nchi na Afrika.

“Kongamano hili linaonyesha umuhimu wa Lugha ya Kiswahili katika Bara la Afrika kwa kuwa ndio

lugha iliyotumika katika Harakati za Ukombozi, nasisitiza Watanzania kutumia Kiswahili ndani na nje ya nchi na lazima Wakalimani wengi wazalishwe ambao watasaidia kutafsiri lugha hii adhimu” amesisitiza Waziri Mkuu Majaliwa.

Waziri Mkuu ameongeza kuwa kuna umuhimu Somo la Historia kufundishwa katika ngazi zote za shule lengo likiwa ni kufundisha vijana historia ya Tanzania, umuhimu na mambo yote ambayo Tanzania imefanya ndani na nje ya nchi ili kulinda tunu na amali za nchi pamoja na kuendelea kulinda amani ya nchi.

Katika Kongamano hilo Mada mbalimbali ziliwasilishwa ikwemo Mchango wa Tanzania katika Ukombozi wa Afrika na Chimbuko la Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Afrika na Umuhimu wake kwa Tanzania, Afrika pamoja na shuhuda mbalimbali za wapigania uhuru.



WAHARIRI WATAKIWA KUSIMAMIA WELEDI KATIKA TAALUMA YA HABARI

Na Richard Mwakafu, DAR ES SALAAM

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa amewataka Wahariri wa Vyombo vya Habari nchini kuzingatia weledi na maadili ya taaluma ya uandishi wa habari ili umma uweze kupata habari sahihi kwa wakati.

Waziri Mkuu ameyasema hayo Mei 20, 2021 Mkoani Morogoro katika Mkutano Mkuu wa 10 wa Jukwa la Wahariri uliobeba Kaulimbiu "Vyombo vya Habari kwa Maendeleo" ambapo amesisitiza kuwa Serikali haitamvumilia mtu yeyote atakayemkwaza Mwandishi wa Habari akiwa katika utekelezaji wa majukumu yake.

"Kaulimbiu yenu ya Vyombo vya Habari na Maendeleo inahamasisha uandishi wa uwajibikaji, Vyombo vya Habari vinapaswa kutambua kuwa

kila habari vinayoandika nyuma yake kuna maslahi ya taifa visipofanya hivyo, upotoshaji unaweza kuigawa nchi yetu, kuhatarisha amani na mshikamano wetu" amesema Waziri Mkuu Majaliwa.

Waziri Mkuu Majaliwa amesisitiza kukamilishwa kwa mchakato wa kuundwa kwa Bodi ya Ithibati ya Habari itakayofanya kazi ya kusimamia maadili ya taaluma ya uandishi wa habari ili kuwezesha uundwaji wa Baraza Huru la Habari ambapo Waziri mwenye dhmana ya sekta hiyo Mheshimiwa Innocent Bashungwa amemhakikisilia Waziri Mkuu kuwa Wizara imeshaanza mchakato kwa kuundwa kwa Bodi na mapendekezo ya majina ya wajumbe wa Bodi yameshawasilishwa kwa ajili ya upekuzi.



WIZARA ZATEKELEZA MAELEKEZO YA WAZIRI MKUU KUHUSU MAAFISA UTAMADUNI NA MICHEZO

Na Shamimu Nyaki, DAR ES SALAAM

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imetekeleza maelekezo aliyoyotoa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mei 21, 2021 wakati akizindua Kongamano la kuenzi mchango wa Tanzania kwenye Ukombozi wa Afrika Jijini Dar es Salaam ya kuitaka Wizara hiyo, Wizara ya Utumishi na TAMISEMI kutatua changamoto za kimuundo kwenye Sekta za Utamaduni na Michezo.

Katibu Mkuu wa Habari Dkt. Hassan Abbasi amekoza kikao hicho kilichoshirikisha Makatibu Wakuu wa Wizara za TAMISEMI na Utumishi, kwenye kikao kazi cha Maafisa Utamaduni na Michezo nchi Tanzania Bara ambapo amesema maelekezo yote yamefanyiwa kazi na kukamilika kilichobaki ni kuandaa nyaraka ili kufanikisha utekelezaji wa maelekezo hayo.

"Kikao hichi kimejadili na kutekeleza maagizo ya Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa aliyotoa Mei 21, ikiwemo kufanya marekebisho ya Muundo wa kada za Maafisa Utamaduni na Michezo, na tayari

kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI na Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora tumeyafanyia kazi" amesema Dkt. Abbasi.

Aidha, Naibu Katibu Mkuu Utumishi, Dkt. Francis Michael amefafanua kuwa muundo ulioboreshwa unamtambua mtaalam mwenye fani nyingine ambazo siyo za michezo lakini ana uzoefu kwenye michezo na amepata mafunzo ya michezo anakuwa na nafasi ya kuwa kwenye kada Afisa Michezo.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI anayeshughulikia Elimu Gerald Mweli amesema Kitengo cha Utamaduni, Sanaa na Michezo kitaundwa na kitatengewa bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya sekta hizo ambapo amesisitiza maafisa hao kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha ili waweze kupimwa utendaji wao kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma.



WAZIRI BASHUNGWA ASISITIZA MAAFISA HABARI KUTOA TAARIFA KWA UMMA

Na Shamimu Nyaki, MBEYA

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Innocent Bashungwa amewaagiza Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano Serikalini kujituma na kufanya kazi yao kwa kasi, ari, weledi na kusistiza atayezembea hatua za kishe-ria zitachukuliwa dhidi yake.

Mhe. Bashungwa ameyasema hayo Mei 24, 2021 Jijini Mbeya katika ufunguzi wa Kikao kazi maafisa hao amesema kikao hicho kiwe chachu ya kuboresha utendaji pamoja kazi na kufanya tathmini ya utekelezaji wa majukumu yao kwa mwaka 2021 ili kutekeleza kauli ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere inayosema "Kujikosoa ni Kujisahihisha."

"Nimeguswa na Kauli Mbiu ya kikao hiki kwa mwaka huu inayosema "Utoaji Taarifa kwa Umma ni Takwa la Kisheria Viongozi wa Umma na Maafisa Habari Tuwajibike. Hivyo, Wizara ninayoisimamia inaendelea kufanya mageuzi makubwa katika kusimamia utoaji wa huduma za habari kwa umma, na hii ni utekelezaji wa Sheria ya Huduma

ya Habari ya Mwaka 2016, na Sheria ya Haki ya Kupata Habari ya Mwaka 2016" amesisitiza Waziri Bashungwa.

Waziri Bashungwa Bashungwa ametumia nafasi hiyo kutoa rai kwa Makatibu Wakuu wa Wizara yake na Ofisi ya Rais TAMISEMI kuhakikisha changamoto zote zinazowakabili maafisa hao ikiwemo kutoshirikishwa kwenye ziara za kutembelea miradi mbalimbali inayotokelezwa na Wizara au Taasisi, baadhi ya Maafisa Habari kuwekwa chini ya Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMMA) ambapo majukumu yake hayapewi kipa-umbele pamoja na kutokuwa na bajeti, vifaa, Inteneti na Simu zinatatuliwa mara moja.

Aidha, amewasisitiza Viongozi wa Wizara, Taasisi, Halmashauri za Wilaya, Manispaa Miji na Majiji kuhakikisha wanatoa ushirikiano kwa Maafisa Habari ili watekeleze majukumu yao ipasavyo.



BASATA, BODI YA FILAMU NA COSOTA ZAAGIZWA KURATIBU VYEMA SUALA LA UHAKIKI WA WASANI

Na Richard Mwamakafu, DAR ES SALAAM

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Innocent Bashungwa ameagiza Taasisi za Baraza la Sanaa la taifa (BASATA), Chama Cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) na Bodi ya Filamu (TBF) kufanya uhakiki wa kazi za sanaa kwa utaratibu anbao haukwamishi kazi za wasanii nchini.

Mhe. Bashungwa amesema hayo Mei 02, 2021 Jijini Arusha ambapo ameeleza kuwa uhakiki unaofanywa na Taasisi hizo lengo lake ni kulinda maadili kwa kuhakikisha maudhui ambayo yapo kinyume na mila na desturi za Mtanzania bila kuathiri ubunifu wa wasanii, maendeleo ya sanaa nchini na kudumaza ukuaji wa ajira.

“Kwa upande wa filamu, uhakiki unasaidia kujua maudhui yaliyopo kwenye filamu husika ili

kuamua ipangiwe daraja gani na unasaidia kuepusha maudhui mabaya ya kuharibu maadili ya jamii yetu yadhhibitiwe kabla ya kufika kwa mtazamaji/msikilizaji” amesema Waziri Bashungwa.

Waziri ameongeza kuwa Wizara inaendelea kupokea maoni na kukutana na wadau ikiwa ni sehemu ya namna ya kuboresha hoja zilizowasilishwa ambazo zitasaidia kuziungani-sha BASATA, COSOTA na Bodi ya Filamu ambapo amewasisitiza wadau ambao hawajawasilisha maoni yao, kuendelea kutoa maoni yatakayosaidia kuwa na Sheria na Kanuni zinazosimamia maudhui ya kazi za Sanaa nchini.



LUGHA YA KISWAHILI NI BIDHAA YA KIMATAIFA

Na Eleuteri Mangi, DODOMA

Serikali imeanzisha mipango ya kimkakati ya kuki-fanya Kiswahili kuwa bidhaa ya Kimataifa ambapo tayari wataalam wa Kiswahili 1318 wamesajaliwa, huku vifaa vya kisasa vya mafunzo ya ukalimani kwa vitendo na matumizi ya TEHAMA katika ukuzaji wa lugha hiyo vilivyogharimu zaidi ya Sh. mil.181 vimenunuliwa.

Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Pauline Gekul ameeleza hayo Mei 07, 2021 Bungeni Jijini Dodoma alipokuwa akijibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima Mbunge wa Singida Mjini alilouliza Je? Serikali ina mpango gani wa kuifanya Lugha ya Kiswahili kuwa bidhaa ya kimataifa ili kuendeleza na kukuza Utamaduni wa Tanzania duniani?

“Tayari tunao mpango wa kufundisha Kiswahili kwa wageni kupitia Balozi zetu nje ya nchi na Serikali imeboresha na kuimarisha mafunzo ya stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni pamoja na kutoa machapisho ya Kiswahili rahisi kwa wataalam wetu” amesema Mhe. Gekul.

Serikali imeanzisha mipango ya kimkakati ya kuki-

fanya Kiswahili kuwa bidhaa ya Kimataifa ambapo tayari wataalam wa Kiswahili 1318 wamesajaliwa, huku vifaa vya kisasa vya mafunzo ya ukalimani kwa vitendo na matumizi ya TEHAMA katika ukuzaji wa lugha hiyo vilivyogharimu zaidi ya Sh. Mil.181 vimenunuliwa.

Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Pauline Gekul ameeleza hayo Mei 07, 2021 Bungeni Jijini Dodoma alipokuwa akijibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima Mbunge wa Singida Mjini alilouliza Je? Serikali ina mpango gani wa kuifanya Lugha ya Kiswahili kuwa bidhaa ya kimataifa ili kuendeleza na kukuza Utamaduni wa Tanzania duniani?

“Tayari tunao mpango wa kufundisha Kiswahili kwa wageni kupitia Balozi zetu nje ya nchi na Serikali imeboresha na kuimarisha mafunzo ya stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni pamoja na kutoa machapisho ya Kiswahili rahisi kwa wataalam wetu” amesema Mhe. Gekul.



SERIKALI KUONGEZA FEDHA KATIKA MAENDELEO YA MICHEZO NCHINI

Na Adeladius Makwega, MANYARA

Serikali inaendelea kupeleka fedha ambazo zina-saidia kuongeza kasi ya kuendeleza na kukuza sekta ya michezo mbalimbali nchini.

Kauli hiyo imetolewa na Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Pauline Gekul wakati wa ufunguzi wa Kongomano la wadau wa michezo mkoani Manyara lililoratibiwa na wilaya ya Babati.

“Kwa sasa fedha za maendeleo ya michezo zinazopelekwa katika ngazi ya chini na shuleni ni

zile ya uendeshaji wa shule zetu za msingi na sekondari na zinatumika kwa manunuzi ya vifaa vya michezo” amesema Mheshimiwa Gekul.

Akizungumza katika kongamano hilo Katibu Tawala wa Wilaya ya Babati, Alpha Matipula amesema kuwa hali ya michezo katika wilaya hiyo ni nzuri kwa kuwa Serikali ya wilaya inashirikiana na wadau wote wa michezo hatua inayosaidia kutatua migogoro ndani ya vilabu vya michezo.



NAIBU WAZIRI PAULINE GEKUL ASISITIZA MICHEZO KUFANYIKA KUANZIA NGAZI YA VIJJI

Na Shamimu Nyaki, MBEYA

Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo Mhe. Pauline Gekul amezitaka Halmashauri zote nchini kusimamia michezo kuanzia ngazi za vijiji ili wananchi waweze kuimarisha afya zao na kukuza michezo kuanzia ngazi ya chini hadi Taifa.

Mhe. Gekul ametoa maagizo hayo Mei 08, 2021 Jijijini Mbeya alipokuwa Mgeni Rasmi katika mashindano ya Riadha ya Tulia Marathon yanayodhaminiwa na Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini ambaye pia ni Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Tulia Ackson.

"Nafahamu kuna asilimia 40 inayotengwa na Halmashauri kwa ajili ya shughuli za maendeleo, natoa rai kwa Viongozi wa Halmashauri kutenga fedha kidogo kwenye hiyo asilimia ambazo zitawezesha shughuli za michezo kwenye maeneo yenu kuanzia ngazi za chini kabisa kwenye vitongoji", amesisitiza Mhe. Gekul.

Mashindano hayo yanalenga kuboresha Miuondombinu ya Elimu na Afya kupitia Taasisi ya TuliaTrust Fund kwenye Jimbo hilo ambapo zinatarijiwa kufikia Watanzania wengi hapo baadae, huku akeleza kuwa mbio hizo zinajumuisha mbio za ndani na nje ya uwanja ambapo kwa hapa nchini zimefanyika kwa mara ya kwanza.

Mshiriki aliyeshika nafasi ya tatu katika mbio za KM 21 ambaye pia ni miongoni mwa Timu ya Taifa ya Riadha inayowakilisha nchi katika mashindano ya riadha yatakayofanyika baadae mwaka huu nchini Japan, Bw. Alphonse Simbu amesema mashindano hayo yamemsadia kufanya mazoezi kwa ajili ya maandalizi ya mashindano yajayo ya Kimataifa ambapo ameahidi kufanya vizuri na kuitanga za nchi.



DKT. ABBASI: SERIKALI KUISAIDIA TIMU YA TAIFA STARS

Na Mwandishi Wetu , DAR ES SALAAM

Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Dkt. Hassan Abbasi amesema Serikali imejipanga kuisaidia Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu (Taifa Stars) kwa kuipatia fedha ili kuongeza ufanisi wa timu hiyo ndani na nje ya nchi.

Dkt. Abbasi amesema hayo Mei 3, 2021 Uwanja wa Benjamin Mkapa Jijini Dar es salaam alipokutana na kufanya mazungumzo na Katibu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) Bw. Alfred Kidau ambapo wamezungumzia namna ya kuiwezesha timu hiyo kwenye maandalizi ya michuano ya awali ya kufuzu Kombe la Dunia yanayotarajiwa kufanyika mwezi Juni hadi Agosti 2021.

“Ili kupata matokeo mazuri wachezaji wetu lazima wawe vizuri kifedha hii itawasaidia kisaikolojia kuweza kupata matokeo mazuri” amesema Dkt. Abbasi.

Ameongeza kuwa Serikali imejipanga kuanzisha vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya michezo ikiwemo kurudisha mchezo wa Bahati Nasibu. Aidha, Bw. Kidau amesema maandalizi yamekamilika huku akiishukuru Serikali kwa jinsi inavyosaida mchakato wa posho za wanamichezo kutolewa mapema.



TAGCO WAMPA TUZO DKT ABBASI KUTAMBUA MCHANGO WAKE

Na John Mapepele, MBEYA

Katibu Mkuu wa Habari wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Dkt. Hassan Abbasi ametunukiwa tuzo na Chama cha Maafisa Habari na Mawasiliano wa Serikali (TAGCO) kwa kutambua mchango na mageuzi makubwa aliyoyafanya kwenye Sekta ya Habari hapa nchini.

Akikabidhi tuzo hiyo kwa Dkt. Hassan Abbasi, Mwenyekiti wa TAGCO, Paschal Shelutete wakati wa kikao cha 16 cha TAGCO kilichofanyika Jijini Mbeya Mei 24, 2021 amesema Dkt. Abbasi ametoa mchango mkubwa akiwa Mkurugenzi wa Idara ya Habari- MAELEZO na Mkuu wa Serikali tofauti na hapo awali.

“Ni katika kipindi hiki ambapo miradi ya kimkakati ya Serikali ilisemewa vizuri zaidi na kufahamika na watu wengi hivyo kuwafanya wananchi kuipenda Serikali yao” Amefafanua Shelutete.

kwa upande wake Dkt. Abbasi amewashukuru

Waandishi kwa kumpa tuzo hiyo na kuahidi kuendelea kuwapa ushirikiano ili waweze kuendelea kutekeleza majukumu wao kika-milifu kwa nafasi yake ya sasa ya Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo.

“Tuendeleo kushirikiana katika cheo hiki kipya cha Katibu Mkuu katika Wizara yetu ambayo ni Wizara muhimu inayogusa umma kwa nyanja ya burudani na huzuni kutokana na Sekta zake” Ameongeza Dkt. Abbasi.

Aidha amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kumwamini na kumrejsha tena kwenye nafasi ya Katibu Mkuu na kuahidi kufanya kazi kwa weledi na bidi ili kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na maelekezo ya Mhe. Rais Samia.



DKT. ABBASI AWASISITIZA MAAFISA HABARI KUZIJUA TAASISI ZAO ILI KUZISEMEA VYEMA

Na Shamimu Nyaki, MBEYA

Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Dkt. Hassan amewataka Maafisa Habari katika Wizara, Mikoa, Halmashauri, Taasisi, Mamlaka na Wakala za Serikali kuzisemea taasisi zao ili zitambulike kwa huduma wanazotoa kwa wananchi.

Dkt. Abbasi amesema hayo alipokuwa akiwasilisha mada inayohusu "Mawasiliano ya Kimkakati ya Serikali katika Zama Mpya za Utekelezaji" Mei 27, 2021 Jijini Mbeya ambayo lengo lake ni kuwajengea uwezo maafisa hao waweze kusemea taasisi zao kimkakati.

"Afisa Habari ni lazima uelewe taasisi yako, maelekezo mapya yanayoingia katika taasisi na namna ya kuyafanyia kazi na mtambue jukumu lenu ni kutoa taarifa kwa kuzingatia Sheria za ndani na nje ya nchi ikiwemo Mkakati wa Kimataifa wa Haki za Kisiasa na Kiraia, hivyo ni lazima muwajibike" amesema Dkt. Abbasi.

Dkt. Abbasi ameongeza kuwa Serikali lazima iaminike na kukubalika kwa wananchi wake, hivyo utoaji wa taarifa utasaidia Serikali kua-miniwa na wananchi, huku akisisitiza ukweli katika kutoa taarifa kwa namna bora, kutumia lugha sahihi na kutatua changamoto kabla wengine hawajaziibua "Lakini lazima Mamlaka ya taasisi ishirikishwe".

Aidha, katibu Mkuu huyo ametoa msisitizo kwa Maafisa Habari kwenda "field" kuona taasisi inatekeleza nini kwa wananchi ili atoe taarifa sahihi.

Kwa upande wake Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Hospitali ya Taifa Muhimbili Bw. Aminiel Eligaesha alitoa pongezi kwa Katibu Mkuu huyo kwa namna alivyofanya mageuzi ya utoaji habari za Serikali kupitia vitengo vya mawasiliano.

KONA YA KISWAHILI

Na Dkt. Resani Mnata
Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Maendeleo ya Utamaduni (Lugha)

KONA YA KISWAHILI KWA LEO INAKUJA NA TAFSIRI YA MANENO MBALIMBALI YANAYOTUMIKA KWENYE MASUALA YA TEKNOLOJIA YA MAWASILIANO

1. Mouse - Kipanya
2. Update - Sahihisha
3. Computer - Tarakilishi
4. Charger - Kimemeshi
5. Device - Kitumi
6. Software - Maunzi Laini
7. Hardware - Maunzi Ngumu
8. Display - Kizinza
9. Word Processor - Kichakata Maneno
9. Install - Sanikisha
10. World Wide Web (WWW) - Wavuti wa Walimwengu
11. Download - Pakua
12. Process - Chakata
13. Browser - Vinjari
14. Mode - Nui
15. Interface - Kikusa
16. Application - Programu Tumizi

KILA MWENYE KUVUMILIA

**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
S.L.P 25, 40470 DODOMA, TANZANIA
Tovuti: www.habari.go.tz**